# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA TANZANIA
## KIPINDI CHA MVUA ZA MASIKA MACHI - MEI 2017





**Imetolewa na:**
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), S.LP 3056 Dar es Salaam, JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Tel. 255 (0) 22 – 2460706-8 ; Fax: 255 - (0) 22 – 2460718 E-mail: met@meteo.go.tz**

**Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Masika kipindi cha Machi-Mei 2017**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua katika kipindi cha Machi - Mei 2017,ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbali mbali wanaohitaji taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na wanyamapori, maliasili na utalii, nishati na maji, mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

**a) Mwelekeo wa msimu wa mvua kipindi cha Machi –Mei, 2017:**

- Katika kipindi cha Machi hadi Mei, 2017 mvua za wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, maeneo ya nyanda za juu Kaskazini mashariki (Arusha, Kilimanjaro na Manyara) pamoja na Pwani kaskazini (Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Tanga na visiwa vya Unguja na Pemba)msimu wa mvua unatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani zikiambatana na vipindi virefu vya ukavu.

- Katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na maeneo machache ya pwani ya Kaskazini mvua zinazoendelea zinatarajiwa kuungana na kuanza kwa msimu wa mvua katika wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Machi, 2017 na kusambaa katika maeneo mengine.

- Kwa upande mwingine, mvua za msimu ambazo zilianza mwezi Novemba 2016 katika maeneo yanayaopata msimu mmoja wa mvua zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika kiwango cha wastani hadi juu ya wastani katika mikoa ya (Dodoma, Singida, Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Mbeya na Iringa).

- Mvua za juu ya wastani zinatarajiwa kuendelea katika mikoa ya (Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na eno la kusini mwa Morogoro (Mahenge).

**b) Athari**

- Pamoja na mabadiliko kidogo yanayotarajiwa katika hali ya maji na malisho, vipindi virefu vikavu ndani ya msimu wa mvua vinaweza kuendelea kusababisha upungufu wa maji na malisho kwa mahitaji ya mifugo na wanyama pori hususan katika maeneo yanayotarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani.

- kutokana na mvua chache zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo, upungufu wa maji unaweza kusababisha milipuko ya magonjwa yatokanayo na ukosefu wa maji salama kwa jamii na matumizi mabaya ya mifumo ya maji taka katika miji.

- Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza na kusababisha mafuriko na athari mbalimbali zikiwemo athari kwa mazao na shughuli za uvunaji mazao.

## (I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA MACHI - MEI 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa iliyopo na inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele II cha taarifa hii), kuna uwezekano mkubwa wa mvua za wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo, mtawanyiko hafifu wa mvua na vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha msimu wa mvua wa Machi hadi Mei, 2017 hususan katika Maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki na pwani ya Kaskazini. Kwa upande mwingine, mvua za msimu ambazo zilianza mwezi Novemba, 2016 katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa msimu wa mvua ni kama ifuatavyo:

1. ***Mvua za Masika 2017 (kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua)***

Msimu wa mvua za Masika, 2017 ni mahususi katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki, pwani ya Kaskazini na visiwa vya Unguja na Pemba, ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Mvua za kipindi cha Machi - Mei 2017 zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo ya Ziwa Viktoria. Maeneo ya pwani ya Kaskazini na Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani. Mvuma zinazoendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Vicktoria na Pwani ya kaskazini zinatarajiwa kuungana na mvua za msimu na kusambaa katika maeneo mengine wiki ya kwanza na ya pili ya Mwezi Machi, 2017. Vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya Pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Matukio ya Vimbunga katika bahari ya Hindi yanatarajiwa kuchangia katika mwenendo wa msimu wa mvua nchini.

***1.1 Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):***

Mvua zinazoendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo ya Kagera na Mwanza zinatarajiwa kuungana na mvua za msimu na kusambaa katika mikoa ya Geita, Mara, Simiyu na Shinyanga katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2017. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

***1.2 Ukanda wa Pwani ya Kaskazini:*** (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro): Maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam na Pwani mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo machache zinatarajiwa kuungana na mvua za msimu na kusambaa katika maeneo mengine (mkoa wa Tanga, visiwa Unguja na Pemba na kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro) wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Machi, 2017. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani. Vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko hafifu wa mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hayo.

***1.3 Nyanda za juu Kaskazini Mashariki:*** (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Mvua katika maeneo hayo zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza na ya pili ya Mwezi Machi, 2017 na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani. Vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko hafifu wa mvua vinatarajiwa katika katika baadhi ya maeneo.

**Mvua za Msimu (Novemba – Aprili) kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.**

Msimu wa mvua za Novemba hadi Aprili ni mahususi kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Magharibi mwa nchi, kanda ya kati, Nyanda za Juu Kusini-magharibi, kusini mwa nchi na pwani ya Kusini). Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuendelea kunyesha na zinazatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi na juu ya wastani katika maeneo ya Mikoa ya Njombe, Songwe, Ruvuma, Mtwara na Lindi pamoja na eneo la Morogoro Kusini (mahenge).

**2.1 Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa):**
Kwa ujumla mvua zinazoendelea zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili 2017.

**2.2 Kanda ya kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):**
Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha katika wiki ya pili hadi ya tatu ya Mwezi Aprili, 2017.

**2.3 Nyanda za juu Kusini Magharibi: (Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe na kusini mwa Morogoro):**
Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2017 na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi kwa kipindi cha msimu kilichosalia. Aidha, mvua za juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Songwe, Njombe, na eneo la Mahenge kusini mwa mkoa wa Morogoro.

**2.4 Maeneo ya kusini na pwani ya kusini (Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara)**
Mvua zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi isipokuwa katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Lindi, ambapo mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa. Msimu wa mvua unatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Aprili hadi wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2017.

| MWELEKEO WA MVUA KIPINDI CHA MACHI-MEI 2017 | WASTANI WA MVUA WA MUDA MREFU (mm) MACHI –MEI (1981-2010) |
|---|---|







*Picha 1 – Ramani ya wastani wa mvua – kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba; Kushoto: Mwelekeo wa mvua katika msimu huu wa Machi hadi Mei 2017.*

***Angalizo:***

*Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani na chini ya wastani.*

**(II) MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya kuongezeka kwa Joto la bahari katikati mwa eneo la Kiikweta la Bahari ya Pasifiki inatarajiwa kufanya joto kufikia kiwango cha wastani katika eneo hili katika kipindi cha Machi –Mei 2017. Ongezeko la joto la bahari linatarajiwa pia katika eneo la Bahari ya Hindi katika kipindi cha Aprili hadi Mei 2017. Joto la bahari la juu ya wastani, katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi katika kipindi cha msimu huu linatarajiwa kusababisha matukio ya vimbunga katika bahari ya Hindi. Aidha, hali ya kuendelea kupoa kwa Joto la bahari ya Atlantiki katika eneo la pwani ya Angola katika kipindi cha miezi ya Aprili na Mei, 2017 inatarajiwa kuongeza msukumo wa hewa yenye unyevunyevu kutoka misitu ya kongo hivyo kuimarisha mifumo ya unyeshaji wa mvua katika baadhi ya maeneo nchini.

**(III) ATHARI NA USHAURI**

**Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Wanyama pori**

Hali ya unyevunyevu katika udongo inatarajiwa kuimarika kiasi kwa uzalishaji wa malisho ya mifugo ukuaji wa mazao na katika katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki(Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na pwani ya kaskazini (Tanga, Dar es Salaam Pwani, kaskazini mwa Morogoro na visiwa vya Unguja na Pemba). Hata hivyo, kuwepo kwa maeneo yanayotarajiwa kupata mvua chache na vipindi virefu vya ukavu kunaweza kuathiri upatinakanaji wa kutosha wa malisho na ukuaji wa mazao. Hivyo, Wafugaji wanashauriwa kuwa na mifugo inayolingania na uwezo wa maslisho yaliyopo pamoja na kuzingatia ushauri wa maafisa mifugo na kilimo kwa maelekezo zaidi katika maeneo yao.

**Maji na Nishati**

Katika maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki, viwango vya maji katika maziwa, mito na mabwawa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani havitarajiwi kupata ongezeko la kuridhisha hivyo, upungufu wa maji kwenye mabwawa unatarajiwa. Inashauriwa kuwa njia mbadala za uzalishaji wa nishati ya umeme zitumike ipasavyo. Wananchi wanashauriwa kuzingatia taratibu za uvunaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali maji katika maeneo hayo. Kwa upande mwingine katika maeneo yanayotarijwa kupata mvua za juu ya wastani hali ya maji inatarajiwa kuimarika katika kipindi husika.

**Mamlaka za Miji**

Kutokana na uwezekano wa vipindi vya mvua kubwa vinavyotarajiwa, Mamlaka za miji pamoja na wananchi wanashauriwa kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanyakazi katika kiwango cha kutosha ili kuepusha maji kutuama na kupelekea mafuriko na uharibifu wa miundombinu. Aidha, hatua hizo zichukuliwe hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani kwa sababu vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza.

**Sekta ya Afya**

Kutokana na uhaba wa maji salama unaotarajiwa kwa shughuli za binadamu ikiwemo usafi wananchi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuzuia milipuko ya magonjwa. Aidha wadau katika Sekta ya Afya pamoja na uma wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

**Menejimenti ya Maafa**

Mamlaka za maafa na wadau wengine wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utunzaji wa mazingira, mipango na hatua za kujiandaa na kukabiliana na majanga yanayoweza kutokea kutokana na mwennendo wa mvua katika msimu unaotarajiwa.

**Vyombo vya habari**

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii. Aidha, jamii nayo inashauriwa kufuatilia na kuzingatia taarifa sahihi za hali ya hewa na mirejeo yake kupitia vyombo vya habari.

Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10 pamoja na za mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.

**Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekoe wa mvua nchini.**

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Dkt. Agnes L. Kijazi
**Mkurugenzi Mkuu**



**Imetolewa na:**
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), S.L.P 3056 Dar es Salaam, JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Tel. 255 (0) 22 – 2460706-8 ; Fax: 255 – (0) 22 – 2460718 E-mail: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz**